

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

## **UJUE SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI**

### **UKOMO WA GHARAMA ZA UCHAGUZI**

*Sheria ya Gharama za Uchaguzi imeweka ukomo wa matumizi ya gharama za uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1), Waziri mwenye dhamana hutoa tangazo katika Gazeti la Serikali linaloonesha ukomo wa matumizi ya gharama za uchaguzi kwa kila jimbo, mgombea urais, chama cha siasa, asasi za kiraia na taasisi za kidini zitakazofanya kazi ya kutoa elimu kwa umma wakati wa uchaguzi. Mgawanyo huo unafanywa kwa kuzingatia masuala yafuatayo:*

- ➔ Tofauti ya ukubwa wa eneo la jimbo;
- ➔ Aina za wagombea;
- ➔ Idadi ya watu katika jimbo; na
- ➔ Miundombinu na mawasiliano.

#### **Wasiliana nasi**

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa  
Viwanja vya Nanenane Nzuguni  
Jengo la Wizara ya Kazi - Mtaa wa Nzuguni A  
S.L.P 2851  
DODOMA

1. Ukomo wa gharama za uchaguzi katika mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya chama cha siasa ni kama ifuatavyo:

- (i) Mgombea urais shilingi bilioni tatu (3,000,000,000/=);
  - (ii) Wagombea ubunge shilingi bilioni tatu (3,000,000,000/=);
  - (iii) Wagombea ubunge viti maalum vya wanawake shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=);
  - (iv) Wagombea udiwani shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=); na
  - (v) Wagombea udiwani viti maalum vya wanawake shilingi milioni mia nne (400,000,000/=).
2. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa chama cha siasa katika kampeni za uchaguzi ni shilingi bilioni kumi na saba (17,000,000,000/=);
3. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni shilingi bilioni sita (6,000,000,000/=);

4. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea wa ubunge katika jimbo la uchaguzi umeanishwa katika sehemu B ya tangazo, ambapo kila jimbo lina ukomo wake;
5. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea wa kiti maalum cha ubunge ni shilingi milioni kumi na moja (11,000,000/=);
6. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea udiwani ni shilingi milioni nane (8,000,000/=) kwa kata ya mjini na milioni sita (6,000,000/=) kwa kata za vijijini;
7. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea udiwani viti maalum, kwa kata ya mjini ni shilingi milioni nne (4,000,000/=) na kwa kata ya kijijini ni shilingi milioni tatu na nusu (3,500,000/=);
8. Kwa upande wa asasi za kiraia na taasisi za kidini zitakazoshiriki katika kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma, ukomo wa matumizi wa gharama za

uchaguzi zitakua kama ifuatavyo: (Kanuni ya 12(1) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi).

- (i) Kwa asasi itakayoshiriki nchi nzima ukomo wake utakuwa shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=);
- (ii) Kwa asasi itakayoshiriki katika ngazi ya jimbo ukomo wake utakuwa shilingi milioni mia moja (100,000,000/=); na
- (iii) Kwa asasi itakayoshiriki katika ngazi ya kata ukomo wake utakuwa shilingi milioni kumi (10,000,000/=).

***Gharama zote za uchaguzi zitakazotumika wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya chama cha siasa zitatokana na chama husika. Kifungu cha 14(1).***

Chama cha siasa au mgombea atakayetumia gharama za uchaguzi zaidi ya ukomo uliowekwa anapaswa kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa akieleza sababu za kufanya hivyo (Kifungu cha 10(2)). Aidha, mgombea au chama cha siasa hakipaswi kutumia zaidi ya asilimia kumi na tano (15%) ya gharama za uchaguzi zinazopaswa kutumika katika eneo husika (Kanuni ya 3 ya Amri za Gharama za Uchaguzi Namba 325 za mwaka 2015).